



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya, S.L.P 113, Iselamagazi,
Shinyanga. Simu/Fax: 0282-986382 Barua pepe: info@shinyangadc.go.tz
Tovuti: www.shinyangadc.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. **SDC.L.2/10/III/170**

16 Desemba, 2025

Mkurugenzi Mtendaji,
Sahara Metacraton Company Limited,
S.L.P 4739,
Dar es salaam.

Yah: **OMBI LA KIBALI CHA KUWEKA MTAMBO WA UCHENJUAJI WA DHAHABU
KATIKA KIJJI CHA MWAKITOLYO**

Tafadhali rejea barua yako yenye Kumb. Na. **SMRCL/001** ya tarehe **14.12.2025** kuhusiana na mada tajwa hapo juu.

2. Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kupitia wataalamu wake imefanya ukaguzi katika kipande cha ardhi kinachoombwa kuendelezwa kwa matumizi ya uchenjuaji wa dhahabu katika Kitongoji cha Nyasubi, Kijiji cha Mwakitolyo tarehe 15.12.2025 na kwa pamoja kukubaliana na ombi lako.

3. Kwa barua hii napenda kukujulisha kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga inakubaliana na ombi lako la kufanya uwekezaji wa mtambo wa uchenjuaji dhahabu katika Kijiji cha Mwakitolyo.

4. Aidha, Halmashauri inasisitiza kufuata Sheria na taratibu zote za nchi katika utekelezaji wa mradi huo ikiwa ni pamoja na;

- a) Kupata Kibali cha mazingira kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).
- b) Kupata Kibali cha Ujenzi (*Building Permit*) kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kwa maendelezo yatakayokusudiwa kufanyika.

- c) Kutekeleza wajibu wenu kwa Jamii (CSR) kama ilivyokubaliwa katika Kikao cha Halmashauri ya Kijiji cha Mwakitolyo na kwa mujibu wa Sheria ndogo za Kijiji.
- d) Kuwezesha Upangaji na upimaji wa ardhi hiyo na baadaye taratibu za utangazaji wa eneo la uwekezaji na umilikishaji kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi, Sura ya 113.

5. Nashukuru kwa ushirikiano wako.


Andrew A. Mitumba

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA**

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
S.L.P. 113
SHINYANGA**